# NOA BONGO
# JENGA MAISHA YAKO

## Maswala ya Jamii- Jinsi ya kuwa mshirika katika siasa

## Kipindi cha kwanza; viongozi huumbwa hawazaliwi

**Mwandishi: Chrispin Mwakideu**

**Mhariri: Andrea Schmidt**

**WAHUSIKA:Mapito(40),Roni(14),Betty(12),Eveline(19), Mkufunzi(35),Samu(14),Vijana(14+)**

UTANGULIZI

Hujambo msikilizaji na karibu katika mfululizo wa vipindi vya Noa Bongo Jenga Maisha yako kuhusu maswala ya jamii – jinsi kijana anavyoweza kuwa mshirika katika siasa. Tunakutana na familia ya Mapito, afisa wa polisi mwenye bidii katika kazi yake. Mke wake aliaga dunia na kumuachia watoto wao watatu awalee pele yake. Eveline ana umri wa miaka 19. Amemaliza shule ya sekondari na anataka kutafuta kazi nyingene mbali na ile ya babake. Ronnie ni kijana wa miaka 14. Ni mchezaji stadi wa kandanda na anataka kuiongoza timu yake. Betty ana miaka 12 tu na ana ndoto ya kuwa muimbaji mashuhuri. Wote wanakabiliwa na changamoto ngumu zitakazowalazimu kutafuta ufumbuzi. Tujiunge na Ronnie na familia yake wakipata kiamsha kinywa katika kisa kwa jina – ´´Viongozi huumbwa, hawazaliwi´´.

## Scene 1: Breakfast table
## Onyesho la kwanza: wakiwa mezani kuamsha kinywa

**SFX: CUTLERY SOUNDS WHEN PEOPLE EAT/DRINK**
**Sauti za vyombo na vifaa vya kulia na kunywia vyasikika**

**1.RONI:** Baba, hujawahi kunieleza. Ni kwanini uliamuwa kuwa afisa

wa polisi?
**2.MAPITO: R**oni, tafdhali niache nifurahie kiamsha kinywa changu. Nafikiri ni mapema mno kuanza mahojiano**.**

**3. BETTY:** Mmmh, nafikiri baba alitaka tuwe salama. Ama sivyo baba ?

**4.MAPITO**: Swadakta malkia wangu, werevu wako umezidi umri wako.

**5.RONNIE**: Lakini si ni kazi ya hatari kuwafukuza wezi, wanyang'anyi wa magari, wezi wa kuchomoa vitu mifukoni mwa watu na hata magaidi siku nzima? (**Roni anafanya milio ya Magari ya Polisi na risasi**)

**6.MAPITO:** Hiyo ndio shida ya vijana wa kileo, munatazama mno filamu zinazowaongopea. Ulimwengu uko tofauti kule nje…

**7.RONNIE**:Baba mimi bado sijaelewa. Ungelikuwa mwanariadha mzuri. Nimeona vyeti vyako ulipokuwa shule ya upili, labda ungeliiwakilisha nchi yetu katika michezo ya Olimpiki na kunyakua nishani ya dhahabu…. hiyo ndiyo ndoto yangu, kucheza kandanda kwa taifa langu na kushinda dhidi ya timu za Ulaya katika mashindano ya kuwania kombe la dunia…

**8.MAPITO**: (**Sternly, fazaa)** Hebu nisikilize kijana! Tena kwa makini sana! Tangu mamako alipoaga dunia, nimejitahidi kwa bidii kuwapa mutakacho na kuhakikisha karo yenu imelipwa. Sitajii uilipe bidii yangu kwa wewe kufukuzana na mpira wa ngozi kuukuu iliyochujuka katika kiwanja kilichojaa vumbi ukidhani umekuwa Pele. Nataka usome na kuwa hakimu, umenielewa? Upo hapo?

**9.RONNIE**: Ndio baba. Sikunuia kukuudhi, nalitaka ushauri wako sababu ningetaka kuwa nahodha wa timu yetu na kuiongoza hadi kufikia fainali lakini sikujuwa ningelifikaje kiwango hicho…

**10.MAPITO**: Nahodha? Alafu kisha? Ha.. alafu? Roni.. sitopendelea wewe upoteze miguu yako. Nimeyaona hayo yakitokea.. Pigo la kumpoteza mama yako linatosha.. Sitostahamili kukuona ukilemaa. Sasa maliza kiamsha kinywa chako na uondoke….

**11:RONNIE**: Lakini baba, napenda kuucheza mpira wa miguu.. na naucheza kwa ustadi.. najuwa nitakapoweka juhudi zaidi nitachaguliwa kukiongoza kikosi chetu.. Tafadhali baba, niruhusu nicheze, japo kwa muhula huu tu hadi fainali…

**12:MAPITO**: Sawa, lakini utacheza muhula huu tu halafu basi.

**13:RONNIE**:Yeeeeah!!!!!! Asante baba, asante baba. Betty, ziwapi njumu zangu na soksi za kuchezea mpira?

**14:BETTY**: Nilizichukuwa nikaziosha, zilikuwa zinanuka fee… Sikuweza hata kupumua. Nimezianika kambani huko nje na njumu zako pia ziko huko huko nje…

**15.MAPITO**:(**laughs at Bettys description, anacheka**) Wavulana siku zote watabakia kuwa wavulana tu!... Roni, kumbuka kuwaongoza wenzako wakati mwengine kunahitaji uwe tayari kuwahudmia na hata kujitolea kwa ajili yao. Na kukujibu swali lako, hiyo ndio sababu niliamua kuwa afisa wa polisi. Betty, hebu nenda umuamshe dadako! Hata kama amemaliza shule ya upili haina maana anatakiwa kulala siku nzima…

**16:NARRATOR: Na huo ni mtazamo kidogo wa familia ya Mapito… baadaye siku hiyo hiyo…**

**<u>Scene 2: At the Football pitch</u>**
**<u>Onyesho la pili; katia uwanja wa mpira</u>**
**SFX: WHISTLE BLOWN BY COACH**
**Kipenga cha mkufunzi kinalia**

**1.COACH: MKUFUNZI**: Ok! Ok! Sawa! Sawa vijana.. tufanyeni duara.. zoezi la leo limekuwa baya zaidi kuliko mazoezi mengine.

Wengi wenu bado muwachoyo na mpira. Nataka mucheze kama timu moja. Timu moja! Nani alieleta mpira?

**2.SAMU**: Ni Roni, yeye alikuwa wa kwanza kufika kiwanjani…

**3.COACH**: **MKUFUNZI:** Sasa huo ndio motisha wa timu ninaotaka kuuona. Hongera Roni. Zoezi la leo limemalizika.. tuungane mikono… Hip hip!

**4.BOYS VOICES**:(**Aloud**) Hurrrah!
**VIJANA:**( **kwa sauti**) huraaaa!

**5.COACH**: **MKUFUNZI:** Roni, hebu subiri kidogo, ningelipenda kuzungumza nawe. Nyie wengine tuonaneni kesho. Na atakayechelewa ni mizunguko mitano kesho.

( **BOYS NOISES FADE OUT SAUTI ZA VIJANA ZAFIFIA**)

Roni, wewe una kipawa na nafasi nzuri katika siku za usoni, lakini hili ni kabumbu, sio tenisi. Ni lazima ucheze na wenzako. Huwezi kila wakati kuwa katika nafasi ya kufunga bao. Ndio maana tuna wachezaji wengine kumi uwanjani… Unanielewa?

**6.RONNIE**: Ndio mkufunzi, nitajizatiti kuleta umoja kuanzia kesho…

7.**COACH**: **MKUFUNZI**: Vyema! Kuna matarajio mengi kutoka kwako. Sasa nenda wenzako wamechoka kukusubiri…

**8.RONNIE**: (**Whistles after them)**
( **awapigia kipenga**) Samu.. jamaa ningojeni…

**9.SAMU**:( **kejeli)** Jamaa yuwaja mchezaji bora wa kimataifa…

**10.RONNIE**: Mwasemaje jamaa? Mwafikiria ni nani atakayenyakuwa ushindi katika mchuano wa leo wa kombe la Afrika?
(**Dead silence Kimya)**

**11.SAMU**: Roni, tunajitoa katika timu.. Hautuhitaji…

**12.RONNIE**: ( **haamini** ) Eti nini? Yaani nyinyi jamaa mwanifanyia mzaha! Hehehehe! Msinichekeshe…

**13:SAMU**: Hatukutanii, tumetoka Roni. Hebu angalia tangu tulipoanza kucheza; walimu wanakupenda wewe tu zaidi. Wasichana wote wanakushangilia wewe.. na ni wazi kuwa mkufunzi atakuteuwa wewe kuwa nahodha…tumepuuzwa, hatuna maana…sisi ni takataka…!

**14:RONNIE**: Nishawaelewa kwa hivyo yote ni kuhusu wasichana? Acheni hizo jamaa!.. Hii ni timu ye… timu yetu! Kila mtu ni mchezaji na ni muhimu. Nisingeliweza kufunga mabao yote yale kama sio juhudi yenu.. nakubali hapo awali nilikuwa na ubinafsi, kiburi, majivuno lakini nawaahidi nitabadilika.. Tafadhalini musijitoe kikosini.. Tunakaribia kuwa mabingwa!!!

**15.SAMU**: Hmmm. Sawa!.. Nafikiri hujakosea... tutabaki kikosini lakini pia wewe utusukumie wale wasichana sio wote uchukuwe wewe...ala?

**SFX: LAUGHTER Kicheko**

**16.RONNIE:** Mnajua kichekeshacho?... Hata sitambui kama wasichana wapo. Lengo langu ni tushinde hii ligi... jamaa Basi Langu hilo linakuja... Kwaherini tutaonana...

**SFX: TRAFFIC NOISES,CARS,BUSES DRIVING KELELE ZA BASI NA MAGARI ZINASIKIKA ZIKIENDA**

**17.NARRATOR: Wahenga walinena, mja hajitoshi… Roni alianza kujifunza hayo.. huku usiku ukikaribia..**

**MUSIC BRIDGE**
**Muziki unasikika…**

**Scene 3:Living Room**
**Sebuleni**

**SFX: KNOCKING ON DOOR Mlango wabishwa**

**1.BETTY**: Ni nani?

**2.RONNIE**: ( **akiigiza sauti ya kuogofya**) ni mimiiiiiii…. Fungua mlangooo… waaa!!!

**3.BETTY**: Wuuuiiii… Roni.. umenishtua!!!

**4.RONNIE**: Hahaha… baba amefika?

**5.BETTY ( akipata pumzi vizuri**) La, hajafika, lakini Eve yuko jikoni… ng'amua mankuli ya usiku ni nini?

**6.RONNIE**: (**SNIFFS) ( akinusa**) Hmmm kwanukia harufu ya samaki wa tilapia aliyekaangwa… hmmmm

**7.BETTY**: Umepata! Na ananukia utamu… kushinda soksi zako si ndio? **( Beti anacheka**) Roni, nahitaji msaada wako.. ningelipenda kuanzisha kwaya… na tuingie mashindano ya uimbaji, lakini unanifahamu mimi nina haya jingi sijui nitaanzaje…

**8.RONNIE**: Pole, siwezi kukusaidia..Wewe unajua uimbaji wangu ni kama wa chura aliyemeza waya wa seng'enge… kwanini usimuulize Evelyn?

**9.BETTY**: Ahaaa ..Sawa kabisa! (**amuita**) Eve.. Eve!

**10.EVELINE**: Sasa kuna nini tena? Usiniulize nikusaidie na kazi zako za shule… huoni nimeshikika na kazi ya kuwaandalia lishe na baba atawasili wakati wowote?

**11.BETTY**: Nimeshamaliza kazi za shule.. nina swali.. nitawashawishi vipi wanafunzi wenzangu darasani ili tuanzishe kundi la uimbaji?

**12.EVELINE**: Ah! Wewe!! Unataka kuanzisha kwaya? Hilo ni wazo zuri! La je baba ushamfahamisha?

**13.BETTY**: Hapana bado. Eeeeh nilitaka nikwambie wewe kwanza halafu wewe ndio umwambie baba…

**14.EVELINE:** Mimi? Kwa nini usimueleze mwenyewe? Ni baba yetu sote na ndiye mzazi pekee tuliye naye.. Usimuogope..Mueleze chochote. Anatupenda na anatutakia kila la heri…
**15.BETTY**: Nafahamu.. Nafahamu, lakini tafadhali.. tafadhali nifanyie hisani hii tu peke yake…

**16.EVELINE**: Betty, unapotaka kuongoza ni lazima uwe na ukakamavu.. na unaanzia hapa nyumbani,...hapa na familia yako. Zungumza na baba, na umueleze umuhimu wake kwako. Na kwa wenzako darsani washawishi ili wakufuate. Waeleze manufaa ya kujiung ana kwaya kwa mfano safari watakazofanya kuzuru sehemu mbali mbali, vipawa watakavyojifunza na kadhalika…

**17.BETTY**: Sijawahi kuwa na mtazamo huo.. unajuwa napenda kuimba, na nikafikiri kila mtu atahisi kama mimi kuhusu uimbaji.

**SFX: DOOR CREAKS OPEN**
**Mlango unasikia ukifunguka**

**18.BETTY: (With a pleasant voice) ( kwa sauti nzuri**) Shikamoo baba……..Naomba nikupokee kofia na koti lako…

**19.MAPITO:** Oh. Kuna nini leo Betty? Ni nadra sana kunitumikia namna hii.. unataka nini leo mama?

**20.BETTY**: Eeeh.. ningependa kuanzisha kwaya katika darasa letu.. Halafu tuingie mashindano ya uimbaji… wajua baba…

**21MAPITO:** Eti nini? Oooh hivyo ni vizuri… siku zote nilikerwa kwa nini hutaki watu waisikie sauti yako ya ninga? Nimekuruhusu binti yangu!

**22.BETTY:** Asante baba.. naenda kumsaidia Eveline kuandaa chakula jikoni…

**23.MAPITO**: Hujambo Roni? Hebu njoo ukae karibu nami… Ehe masomo yalikuwaje leo?

**24.RONNIE**: Magumu! Mkufunzi wangu ananishinikiza sana na daima ananiona na makosa… Halafu wachezaji wenzangu pia walitaka kukihama timu yetu… ilinibidi kuwasihi wasifanye hivyo kwa kuwa tumeingia fainali…hata nafikiri wenzangu wanataka kunisaliti..

**25.MAPITO**: Sishangai! Unajuwa unapoanza kufanikiwa, hapo ndipo unapojua marafiki wako halisi ni akina nani… Usijali, lenga shabaha yako…unaposukumwa kutoka nyuma juwa uko mbele…

**26.BETTY**: Chakula tayari

**27.MAPITO**: (**Yawns**)At long last.i was beginning to wonder what was cooking that long.

**MAPITO:** ( **akienda miayo**) Aah afadhali kwani nilikuwa nimeanza kujiuliza munapika nini kinachochukua muda mrefu hivyo. Chakula hakiivi!!!

**Mwisho wa kipindi cha kwanza**

**MSIMULIZI:**

Huo msikilizaji ndio mwanzo wa hadithi yetu kuhusu ndugu watatu wenye azma ya kutimiza ndoto zao. Ndoto ya Eveline ni ipi? Je Roni atachaguliwa kuwa nahodha wa timu yake? Na je Betty atashinda hisia za kuona aibu na kuanzisha kwaya? Jiunge nasi wiki ijayo upate kujua. Kumbuka unaweza kukisiliza tena kipindi hiki kwenye mtandao wa internet. Tovuti yetu ni: www.dw-world.de/lbe